TANGAZO LA SERIKALI Na.1008 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA ULINZI WA UMMA YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ulinzi wa Umma ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye anaishi ndani ya eneo la Halmashauri na ana umri wa kuanzia miaka kumi na nane;

"kaya" maana yake ni baba, mama na watoto wenye umri usiozidi miaka kumi na nane au mtu yeyote aliyetimiza umri wa kuanzia miaka kumi na nane awe na mtoto au bila mtoto.

Wajibu wa kila mkazi kushiriki katika ulinzi wa umma

4.-(1) Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika kushiriki katika shughuli za ulinzi wa umma kama zitakavyoratibiwa na uongozi wa kata, mtaa, Halmashauri au Jeshi la Polisi kwa kadri itakavyofaa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mkazi atawajibika kufanya moja ya mambo yafuatayo:

(a) kushiriki ulinzi yeye mwenyewe kwa muda usiopungua saa nane katika muda wa saa ishirini na nne mfululizo; au
(b) kaya yake kuchangia ada ya ulinzi kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Serikali ya Mtaa, Kamati ya Maendeleo ya Kata au Halmashauri kulingana na hali halisi kwa ajili ya kugharamia shughuli za ulinzi, kukodisha kampuni binafsi ya ulinzi au kununua vifaa vya ulinzi.

Kuanzisha kikundi cha ulinzi

5. Kikundi cha ulinzi kitaanzishwa katika kila kata au mtaa ndani ya Halmashauri kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika eneo la kata au mtaa kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi.

Kiongozi wa kikundi cha ulinzi

6. Kila kikundi cha ulinzi kitakuwa na kiongozi atakayetambuliwa kama Kamanda wa kikundi ambaye atateuliwa kutoka miongoni mwa watu wanaounda kikundi cha ulinzi cha kata au mtaa.

Wajibu wa kamanda kuandaa orodha ya wakazi

7. Kila kamanda wa kikundi atatakiwa kuwa na orodha ya wakazi wote wanaostahili kushiriki katika shughuli ya ulinzi ndani ya kata au mtaa na orodha hiyo itahifadhiwa katika daftari maalum na kutunzwa katika ofisi za kata au mtaa.

Wajibu wa kuwasilisha taarifa

8. Kila kamanda wa kikundi cha ulinzi atawajibika kusimamia kikundi kitakachokuwa zamu kwa siku husika na kuwasilisha orodha ya walinzi waliopo zamu katika ofisi ya kata au mtaa ambapo kikundi cha ulinzi kipo.

Makosa

9. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-
(a) bila sababu za msingi hatashiriki katika shughuli za ulinzi;
(b) atashawishi mtu yeyote kutoshiriki katika shughuli za ulinzi; au
(c) atamsaidia mtu yeyote kukwepa kushiriki shughuli za ulinzi.

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi elfu hamsini na kisichozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoambatanishwa kwenye Jedwali la Ndogo hii.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 217 la 2008

12. Sheria Ndogo za Ulinzi wa Umma za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala za Mwaka 2008.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ………. mwaka ……….…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ulinzi wa Umma ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, NAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi…………. ambayo ni ada ya ulinzi ninayodaiwa pamoja na kiasi cha shilingi ……………. kama faini ya kufifilisha kosa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina………………………………. Saini………………………

MBELE YA MKURUGENZI:
Jina:……………………………..……………………
Saini………………………..…………………………..………
Tarehe………………………………………………………….

Lakiri ya Jiji la Dar es Salaam imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutao wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam uliofanyika tarehe 6/3/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

JOMAARY MRISHO SATURA,
*Mkurugenzi wa Jiji,*
*Halmashauri ya jiji,*
*Dar es salaam*

MHE. OMARY KUMBILAMOTO,
*Msahiki meya,*
*Halmashauri ya jiji,*
*Dar es salaam*

L.S

**NAKUBALI**,

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*

Dodoma,
29 Agosti, 2024